Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 04 Issue: 01 | July-2025

EAJK

# Athari ya Uraibu wa Dawa za Kulevya kwa wanajamii kupitia Nyimbo za Kizazi Kipya Mtandaoni

Author(s)
Stephen Muyundo Ndinyo [1]; Ernest Sangai Mohochi [2]; Joseph Juma Musungu [3]
Main author email: muyundos@gmail.com

(1.2.3) Kibabii University, Kenya.

**Cite this article in APA**
Ndinyo, S. M., Mohochi, E. S., & Musungu, J. J. (2025). Athari ya uraibu wa dawa za kulevya kwa wanajamii kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. *Eastern Africa journal of kiswahili, 4* (1), 55-63.
https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.764

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 2025-05-21
Accepted: 2025-06-20
Published: 2025-07-21

Scan this QR to read the paper online

**Copyright:** ©2025 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Suala la dawa za kulevya ni mojawapo ya masuala ibuka lenye athari kubwa katika jamii huku mtandao ukichangia hali hii. Makala haya yalichunguza madhara yake yalivyosawiriwa katika mapambano dhidi ya mihadarati kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Kazi hii iliongozwa na Nadharia ya Athari ya Vyombo vya Habari iliyoasisiwa na McLuhan's (1964). Muundo wa kithamano mkabala wa kiutendaji ulitumika. Mbinu ya ukusanyaji data iliyotumika ni uchanganuzi wa yaliyomo. Mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kukusanya data mtandaoni. Umma lengwa ulihusisha nyimbo za kizazi kipya na mtandao. Mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi ilitumika kuchagua nyimbo za kizazi kipya za Kiswahili, suala la dawa za kulevya na mtandao wa *You Tube*. Kisha, usampulishaji wa kitabaka ulitumika utabakisha nyimbo kidhima na kwa kurejelea aina tofauti ya mihadarati iliyosawiriwa. Jumla ya nyimbo tano na mtandao mmoja ulilengwa. Kazi hii ililenga kupata data ya kimaelezo iliyowasilishwa kwa kutumia maelezo ya kifafanuzi, mijadala, mifano na dondoo. Matokeo ya kazi hii ni kwamba nyimbo za kizazi kipya ziliangazia athari zake kwa jamii, familia na waraibu wa dawa tofauti za kulevya kama njia mojawapo ya kuhamasisha jamii katika mapambano dhidi ya mihadarati. Makala haya yanapendekeza mitandao mbalimbali tofauti na ule wa *YouTube* kutafitiwa kwa kurejelea madhara ya mihadarati. Pili, uchunguzi wa athari ya uraibu wa mihadarati kwa kurejelea nyimbo nyinginezo mbali na zile za kizazi kipya. Hatimaye, madhara ya mihadarati pia zitafitiwe katika tanzu nyingine za fasihi pepe kama vile vichekesho, filamu na vipindi vya runinga.

**Maneno muhimu:** Athari, mapambano, mihadarati, mtandao, nyimbo za kizazi kipya.

**UTANGULIZI**

Uraibu wa dawa za kulevya umetokea kuwa mwiba katika jamii tangu jadi kwa kuwadhuru wanajamii kila uchao. Suala hili limeendelea kuwa tatizo kubwa sana katika siku za hivi karibuni. Maendeleo ya kasi ya mtandao yamechangia katika kurahisisha upitishaji wa habari sio tu katika kuendeleza uraibu huu ila pia katika mapambano yake. Dawa za kulevya ni kemikali au vitu vinavyobadilisha hali ya mwili au akili ya binadamu huku vikiweza kusababisha utegemezi wa kimwili au kiakili na zinaweza kuwa ni halali au haramu na zitumiwapo kwa njia isiyosahihi zaweza kuathiri afya ya akili, mwili na maisha ya kijamii ya mtu (United Nations Office on Drugs and Crime, 2016)

Dawa za kulevya zilikuwa na athari mbalimbali katika jamii kutokana na uraibu wake katika jamii. Kwanza kabisa, zilisababisha waraibu wake kuwa wendawazimu, zilisababisha vifo vya waraibu wengi wakiwa vijana, kuwa chanzo cha magonjwa mbalimbali katika mwili wake mraibu ya kiafya kama vile uraibu, matatizo ya afya, matatizo ya kiakili, maambukizi ya Ukimwi, saratani inayohusiana na homa ya ini na uharibifu wa maini, matumizi ya dawa kupita kiasi na vifo vya mapema (Mbeere, 2022; Nyamemba, 2015 & World Drug Report (WDR), 2022). Madhara haya yalikuwa mwimba katika jamii katika karne ya 21.

Nyimbo za kizazi kipya ni zenye mahadhi ya mchanganyiko wenye vionjo vyenye asili ya Karibi, Marekani na sehemu nyingine duniani (Jumbe, 2015). Nchini Kenya, zilichipuka katika miaka ya 1990 na sasa ni maarufu sana miongoni mwa vijana ni zenye asili kutoka mji wa *Bronx* huko *New York* na Wamarekani wenye asili ya Kiafrika katika mwaka wa 1970. Nyimbo za kizazi kipya mtandaoni zimeangazia suala hili la uraibu wa mihadarati kwa kusawiri madhara mbalimbali ya dawa za kulevya kupitia video zake za mtandaoni. Usawiri huu ulilenga kuwatahadharisha watazamaji dhidi ya uraibu wa mihadarati katika jamii. Hivyo basi, nyimbo za kizazi kipya zilipinga uraibu wa dawa za kulevya katika mapambano dhidi ya mihadarati katika nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

Makala haya yaliangazia jinsi nyimbo za kizazi kipya mtandaoni zilivyochangia katika vita dhidi ya matumizi ya mihadarati. Mjadala wa kina ulikuzwa kurejelea juhudi za watunzi wa nyimbo teule za kizazi kipya katika kusawiri athari tofauti za uraibu wa dawa za kulevya katika mapambano dhidi ya mihadarati kupitia nyimbo zao za kizazi kipya mtandaoni. Makala haya yalihusisha sehemu ya utangulizi, sehemu ya mapitio ya maandishi kuhusu kazi mbalimbali za fasihi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Kisha, sehemu ya nadharia na ile ya mbinu za utafiti ilirejelewa. Hatimye, sehemu ya matokeo ya makala na ile ya hitimisho na mapendekezo zilijadiliwa.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Athari ya Mihadarati katika Kazi za Fasihi katika Mapambano dhidi ya Dawa za Kulevya**

Sehemu hii ilishughulikia uhakiki wa maandishi kwa kurejelea tafiti za jumla kuhusu athari ya mihadarati katika nyimbo teule za kizazi kipya mtandaoni katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Kazi hizi zilirejelea nyimbo mbalimbali na vyombo vya habari tofauti kuhusu suala hili ibuka la mihadarati kwa jumla. Vyombo vya habari kutokana na maendeleo ya kiteknolojia vina nafasi kubwa katika mapambano dhidi ya uraibu wa dawa za kulevya katika karne hii ya 21. Maendeleo katika teknolojia ya mawasiliano yameenea kote kote ulimwenguni na kuwaunganisha na kuwahamasisha wana jamii. Mtandao umerahisisha kusambazwa kwa machapisho ya magazeti, makala na vitabu. Mwishowe, kupeperushwa kwa vipindi vya redio na runinga, filamu na miziki kwenye radio na runinga na mitandao mbalimbali.

Kwanza kabisa, vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika kuhamasisha jamii. Baadhi ya miziki ya *Gengetone* ilihamasisha kuhusu hatari ya matumizi ya mihadarati katika redio na runinga (Koech, 2021). Maoni ya Koech (2021) ni faafu kwa kazi hii kwa kuwa yalidhihirisha kwamba vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika kuhamasisha jamii. Hatari ya matumizi ya dawa za kulevya vilevile, ilibainika katika nyimbo za kizazi kipya mtandaoni katika mapambano dhidi ya mihadarati.

Suala hili la dawa za kulevya pia limeangaziwa katika nyimbo tofauti katika vyombo vya habari. Nyimbo mbalimbali katika *I- Tunes, You Tube* na runinga zilisawiri suala hili la mihadarati. Kwanza kabisa vyombo vya habari vilikuwa na athari katika kusikiliza na kupokea nyimbo (Kuyucu, 2015). Maendeleo katika vyombo vya habari yameathiri njia za kitamaduni za kusikiliza nyimbo miongoni mwa vijana kama vile redio na kujenga jukwaa jipya la kusambaza, kupenda, kutoa



DRAFT

mrejesho, kupakua, kusikiliza na kutazama nyimbo kwenye mtandao. Maoni haya ya Kuyucu (2015) yalituongoza kwa kutafitia mtandao kwa vile sasa ni jukwaa kubwa katika jamii hasa katika kusikiliza na kutazama muziki, ukiwemo ule unaolenga dawa za kulevya.

Kwa upande mwingine Ruhweza (2018) na Kuyucu (2015) walishughulikia suala la mihadarati katika vyombo vya habari. Runinga ya NBS ilikuwa na athari kubwa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kule Uganda (Ruhweza, 2018). Pia, aliangazia changamoto mbalimbali katika vita dhidi ya matumizi ya mihadarati katika runinga ya NBS. Kwa kuzingatia maoni yao Ruhweza (2018) na Kuyucu (2015) ilibainika wazi katika kazi hii kwamba vyombo vya habari hususan mtandao vilikuwa na nafasi kubwa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Nyimbo zilizosikizwa na vijana zilikuwa na madhara makubwa kubwa kwa wale waliohusiana nao. Vijana wanaosikiliza nyimbo zinazohusiana na dawa za kulevya wana uwezekano mkubwa wa kujihusisha na wenzao wanaotumia dawa hizo za kulevya (Motyka & Ahmed, 2019). Hivyo basi, kwa kuzingatia maoni yao Motyka et al. (2019) ni dhahiri kwamba uhusiano upo kati ya kusikiliza nyimbo zinazorejelea mihadarati na matumizi ya dawa halali na haramu. Hali hii ilibainika katika kazi hii kwa kusikilizwa na kutazamwa kwa nyimbo za kizazi kipya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Nyimbo zina uhusiano wa moja kwa moja na matumizi ya mihadarati. Kusikiliza kwa aina tofauti ya nyimbo kulihusiana na matumizi ya aina tofauti za dawa za kulevya. Kusikiliza kwa nyimbo za kufoka kulihusiana moja kwa moja na unywaji wa pombe (Chen, Miller, Grube, & Waiters, 2006). Mbali na unywaji wa pombe, matumizi ya bangi ambayo yalikuwa sawa kwa kuhusiana na nyimbo za kufoka na zile za raggae (Chen et al., 2006). Hata hivyo, makala haya yalidhihirisha uhusiano wa nyimbo za kizazi na uraibu wa mihadarati katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mihadarati ilikuwa na athari mbalimbali katika jamii ya kisasa katika karne ya 21. Kwanza kabisa, uraibu wa mihadarati ulisababisha waraibu wake kuwa wendawazimu (Mbeere, 2022). Dawa za kulevya ziliwaelekeza vijana kwa kaburi huku taifa likiangamia kwa kukosa viongozi wa kesho (Nyamemba, 2015). Kifo pia kilitokea kwa wimbo *Tupatupa* kwa mzee Tupatupa kugongwa na lori aliposimama barabarani kwa sababu ya ulevi. Madhara tofauti ya mihadarati yalibainika moja kwa moja katika nyimbo za kizazi kipya kifo kikiwa mojawapo.

Majukumu ya wanaume na wanawake yalibainika moja kwa moja katika jamii za kiafrika. Jamii iliyofuata mfumo dume, mwanamke alifanya majukumu ya ndani ya nyumba wakati mwanamke akifanya majukumu ya nje (Massoud, 2018). Majukumu ya mwanamume yalikuwa ni kuchunga mifugo, kulinda jamii na kukimu familia (Musembi, 2016). Bwana harusi alishauriwa kuwa ana jukumu la kuwatembelea wazazi wakwe, kuwaheshimu na kuwatunza kwani ndio waliompatia ubavu wake (Norah, 2017). Jukumu la mume lilikuwa ni kuikimu familia yake vyema. Hali hii ilibainika huku waraibu wa mihadarati wakitelekeza majukumu yao katika nyimbo za kizazi kipya. Wanawake nao walikuwa na jukumu la kuzaa watoto, kuwapikia, kuchota maji, kutafuta kuni, kulima, kupalilia na kuvuna mazao miongoni mwa majukumu mengine (Musembi, 2016). Mwanamke pia alichorwa kama asiyetambua jukumu lake katika jamii kwa kujiremba na kujitazama kiooni (Mukandabvute & Gores, 2021).

Uraibu wa dawa za kulevya ni tishio kubwa kwa maendeleo ya kiuchumi katika taifa lolote lile. Uraibu wa dawa za kulevya ulichangia kutofika kazini, kubadilika kwa tabia za mhusika kazini na kupungua kwa viwango vya utendakazi miongoni mwa wafanyikazi (Kaniki, 2019). Wafanyikazi wengi ambao ni waraibu wa *Pombe* walikosa kwenda kazini mara kwa mara, walikuwa na utendakazi wa chini, maroeroe ya ulevi, msongo wa mawazo, changamoto za kifedha na athari za kiafya (Kaithuru, Stephen, & Wanjiru, 2015). Kazi hii ilidhihirisha hali hizi ikiwemo kufutwa kazi katika nyimbo za kizazi kipya katika mapambano dhidi ya mihadarati mtandaoni.

Matumizi ya dawa za kulevya yalikuwa chanzo cha magonjwa mbalimbali katika mwili wake mraibu. Madhara ya kiafya ya dawa ni kama vile uraibu, matatizo ya afya, matatizo ya kiakili, maambukizi ya Ukimwi, saratani inayohusiana na homa ya ini na uharibifu wa maini, matumizi ya dawa kupita kiasi na vifo vya mapema (World Drug Report, 2022). Makala

haya yalionyesha waraibu katika hali hii katika nyimbo za kizazi kipya kuhusiana na mihadarati.

Suala la uasherati lilichangiwa na masuala mbalimbali, matumizi ya dawa za kulevya ikiwa mojawapo. Asilimia sitini nukta tano (60.5%) ya watafitiwa walikiri kuwa walipolewa walishiriki ngono bila kinga (Atwoli et al., 2011). Kwa upande mwingine wenzao waliokuwa asilimia sitini na mbili nukta tano (62.5%) wakijutia kushiriki ngono kutokana na kuwa walevi chakari keshoye (Atwoli et al., 2011). Kazi hii ilibainishi jinsi suala hili la uasherati katika nyimbo za kizazi kipya kuhusiana na uraibu wa mihadarati.

### Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Athari ya Vyombo vya Habari (Mass Effect Theory). Nadharia hii iliasisiwa na Marshall McLuhan's katika mwaka wa 1964. Nadharia hii hueleza jinsi ambavyo vyombo vya habari huathiri mitazamo na machukulio ya hadhira yake. Athari ya vyombo vya habari ni majibu ya kijamii au kisaikolojia ya mtu binafsi, kikundi kidogo, shirika au jamii kama matokeo ya kuwa kwa hali fulani au usindikaji vinginevyo kurejelea habari katika vyombo vya habari.

Nadharia ya Athari ya Vyombo vya Habari ina mihimili mitano (Valkenburg, Peter & Walther, 2016). Mihimili hii ni kama ifuatavyo; Kwanza, kuwepo na uteuzi wa matumizi ya vyombo vya habari. Pili, ni kuwa vyombo vya habari vinatabirika. Tatu, ni kwamba vyombo vya habari ni vya athari isiyo ya moja kwa moja. Nne, ni athari ya vyombo vya habari ni yenye masharti. Hatimaye, mhimili wa tano ulikuwa athari ya vyombo vya habari ni ya kuenea. Moja kati ya mihimili mitano ya nadharia hii ulitumika katika kazi hii. Mhimili huu ni wa nne unaosema kwamba, athari ya vyombo vya habari ni yenye masharti. Mhimili huu ulitumiwa kuchanganua data kuhusu madhara ya uraibu wa mihadarati kwa wanajamii kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

## MBINU ZA UTAFITI

Makala haya yalitumia muundo wa kithamano mkabala wa kiutendaji. Mkabala huu ni uchunguzi wa kitaratibu unaolenga kupata suluhu mwafaka kwa matatizo wanayokumbana nayo wanajamii kila siku (Stringer, 2007). Muundo wa kiutendaji ulilenga suala ibuka la dawa za kulevya lililohitaji suluhu la moja kwa moja katika jamii.

Makala haya yalilenga kushirikisha nyimbo za kizazi kipya, mtandao wa *YouTube,* suala ibuka la mihadarati na nyimbo za lugha ya Kiswahili zililengwa katika mapambano haya dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni. Usampulishaji ni mchakato wa kuteua sampuli kutoka katika kundi lengwa (Kothari, 2004). Makala haya yalishirikisha usampulishaji wa kimaksudi na ule wa kitabaka. Usampulishaji wa kimakusudi ulitumika kuchagua nyimbo za kizazi kipya mtandaoni kwa kurejelea vigezo mbalimbali. Vigezo hivi vilikuwa ni kigezo cha suala ibuka la mihadarati kutokana na madhara yake katika jamii. Kisha, nyimbo za kizazi kipya za lugha ya Kiswahili pekee kwa sababu ya umaarufu wake nchini Kenya. Mwishowe, mtandao wa *YouTube* ulisampulishwa kimaksudi kwa kuwa jukwa la mtandao lenye watazamaji wengi hususan vijana nchini Kenya. Usampulishaji wa kitabaka uligawa nyimbo za kizazi kipya katika matabaka kidhima kwa kusawiri suala la dawa za kulevya ili kubainisha mchango mbalimbali wa dawa za kulevya mtandaoni. Aidha, nyimbo pia zilitabakishwa kwa matabaka tofauti kwa kurejelea dawa za kulevya ili kusawiri mapambano dhidi ya mihadarati mbalimbali katika jamii. Jumla ya nyimbo tano za kizazi kipya mtandaoni zilishirikishwa katika kazi hii.

Mtafiti alizingatia uyakinisho na alipunguza au kukoma kabisa kudhihirisha upendeleo (Ogechi, 2024). Vile vile, alihakikisha kuwa data alizokusanya na matokeo yalihifadhiwa kwa siri (Kristin, 2002). Aidha, matokeo yalitumika tu kwa minajili ya utafiti uliokusudiwa wala sio kwa sababu zingine zozote zile (Burns, 2000). Kisha, uchapishaji wa matokeo ya utafiti huu ili kukuza utafiti na taaluma, na wala si kujikuza tu kibinafsi kwa mtafiti (Ogechi, 2024). Mwishowe, tulitambua kazi za wataalam wengine kwa kuwanukuu na kuwajumuisha katika marejeleo ili kuepuka wizi wa kitaaluma (Resnik, 2021).

## MATOKEO YA UTAFITI

### Athari ya Uraibu wa Mihadarati katika Jamii kupitia Nyimbo za Kizazi Kipya Mtandaoni

Dawa za kulevya zina madhara tofauti katika jamii kutokana na matumizi yake. Dawa tofauti huwaathiri wahasiriwa kwa njia tofauti katika jamii. Madhara haya yalikuwa ya moja kwa moja kwa waraibu, familia zao,

marafiki na jamii kwa ujumla. Nyimbo za kizazi kipya zilitumika kupinga matumizi ya dawa za kulevya kwa kuangazia madhara yake katika jamii. Nyimbo hizi zililenga kuwahamasisha wanajamii ili waepukane na uraibu wa mihadarati ili kuepukana na madhara yake katika jamii.

Nyimbo za kizazi kipya ziliangazia athari mbalimbali za mihadarati katika jamii. Nyimbo hizi nne (4) ni wimbo *Mihadarati* wao Stivo Simple Boy na ule wake Domani Munga na SewerSyda, *Pombe* wake Rose Muhando na wimbo *Bangi* wake Nduati. Kwanza kabisa, uraibu wa dawa za kulevya umeathiri jamii kwa kiwango kikubwa mno. Waraibu katika jamii wamepoteza urazini wao kutokana na matumizi ya mihadarati katika nyimbo tatu (3) za kizazi kipya. Nyimbo hizi ni wimbo *Mihadarati* wake Stivo Simple Boy na ule wa Rusty Gee na *Bangi* wake Nduati.

Kwanza kabisa, uraibu wa matumizi ya dawa za kulevya ulikuwa na madhara kwa wanajamii. Waraibu haswa vijana hupoteza urazini wao baada ya kutumia mihadarati kwa kipindi kirefu kama ilivyojitokeza katika kazi yake Mbeere (2022) aliporejelea matini teule za fasihi ya watoto ya Kiswahili. Tazama ubeti wa pili mshororo wa nne katika wimbo huu wa Stivo Simple Boy uitwao *Mihadarati*;

> Wanapoteza wakati hawana Habari
> Ukivuta mihadarati inaharibu akili, inaharibu paka mwili

Wimbo huu unaangazia matumizi ya mihadarati huvuruga akili za waraibu wake. Vijana wanapoteza muda wao mwingi kwa matumizi ya mihadarati bila kufahamu kuwa uraibu huo huchangia wendawazimu katika jamii. Hali hii pia ilijitokeza katika ubeti wa pili mshororo wa kwanza na wa pili katika wimbo *Bangi* wake Nduati;

> Yo, naishi mtaa youths wapepagawa huku,
> Wengine wameachilia wire juu ya drugs, guns, violence

Wimbo huu *Bangi* unashikilia kwamba vijana wengi katika jamii wameathirika kwa kuwa wendawazimu kutokana na matumizi ya bangi katika jamii. Wendawazimu huu unatokana na matumizi ya kupindukia ya bangi kama moja wapo ya mihadarati ambayo inasababisha wendawazimu katika jamii.
Kisha suala hili la kupoteza urazini pia lilijitokeza katika wimbo *Mihadarati* wake Rusty Gee katika ubeti wa kwanza mshororo wa kumi na tano kama ifuatavyo;

> …Itakufanya uwe chizi,
> machizi maskani sisi ni machipukizi

Mshororo huu unashadidia ujumbe katika nyimbo *Mihadarati* wake Stivo Simple Boy na *Bangi* wake Nduati. Vijana hawa wanapoteza urazini wao kutokana na matumzi ya mihadarati katika jamii. Nyimbo hizi tatu (3) zimelenga kuwatahadharisha wanajamii haswa vijana kuepukana na matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Hivyo basi, nyimbo hizi zilichangia katika vita dhidi ya dawa za kulevya kwa kuangazia athari yake ili kuwaonya wanajamii dhidi ya matumizi haya ya mihadarati.

Dawa za kulevya pia zilichangia kupoteza kwa uhai kwa wale wanaozitumia kupindukia. Unywaji pombe wa kupindukia umehusishwa na vifo, karibu vifo milioni tatu iliyowakilisha asilimia tano nukta tatu (5.3%) vilihusishwa moja kwa moja na unywaji *Pombe* wa kupindukia katika ulimwengu mzima (World Health Organization, 2019). Wimbo huu wa *Mihadarati* wake Rusty Gee uliangazia janga kubwa katika jamii kupitia korasi yake kama ifuatavyo;

> Wapo wengi tumewapoteza sana,
> chanzo kubwa, mihadarati,
> Taifa langu linalia sana, ulevi bado ni changamoto x4

Korasi hii iliangazia kifo cha watu wengi katika taifa kwa sababu ya matumizi ya mihadarati. Maangamizi haya ya wananchi yalisababisha majonzi na kilio katika taifa nzima yaliyosababisha kwa sababu ya matumizi ya mihadarati. Hali hii pia ilibainika katika ubeti wa pili mishororo ya pili na nane kwa wimbo wao Domani Munga naye SewerSyda uitwao *Mihadarati*;

> …mpaka kuna chokoch aliuawa…
> …tuliregret alikufa kaa amejifunika carpet chini ya bed…

Mishororo hii ilionyesha kwamba uraibu wa dawa za kulevya ulichangia kifo katika jamii. kwanza kabisa,

chokora anauliwa kwa sababu ya uraibu wa mihadarati. Kisha, kijana mwenzake alipatikana akiwa amejifunika zulia chini ya kitanda. Hivyo basi, ni bayana kuwa uraibu wa mihadarati ulisababisha vifo katika jamii. Wanajamii wanashauriwa kujiepusha na uraibu wa dawa za kulevya ili kutokuwepo na vifo haswa vya vijana katika jamii.

Matumizi ya dawa za kulevya yalikuwa na madhara katika utendakazi wa waraibu wake katika jamii. Matumizi ya dawa za kulevya yalikuwa na athari hasi kwa utendakazi wa wafanyikazi katika kampuni za bima (Kaniki, 2019). Uraibu wa mihadarati ulichangia kutofika kazini, kubadilika kwa tabia za wahusika kazini na kupungua kwa viwango vya utendakazi miongoni mwa wafanyikazi katika kampuni za bima nchini Kenya (Kaniki, 2019). Wafanyikazi wengi ambao ni waraibu wa *Pombe* walikosa kwenda kazini mara kwa mara, walikuwa na utendakazi wa chini, maroeroe ya ulevi, msongo wa mawazo, changamoto za kifedha na madhara ya kiafya (Kaithuru et at., 2015).

Nyimbo tatu (3) za kizazi kipya ambazo ni wimbo *Mihadarati* wake Rusty Gee na ule wa Stivo Simple Boy zilisawiri hali hii. Dawa za kulevya zilikuwa na athari mbalimbali kwa utendakazi wa waajiriwa kazini kama ilivyojitokeza katika nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Hali hii ilibainika katika ubeti wa kwanza mshororo wa saba katika wimbo wake Rose Muhando uitwao *Pombe*;

> …Pombe imesababisha mume kufutwa kazi…

Mshororo huu unabainisha madhara ya uraibu wa pombe kwa utendakazi kwa mume kupoteza kazi. Mwanamume huyu anafutwa kazi kutokana na ulevi wake uliomfanya kuibiwa stakabadhi za kazi katika klabu na warembo wawili. Utepetevu huu unamkasirisha bosi wake na hivyo anaachishwa kazi.
Uraibu wa dawa za kulevya uliathiri wafanyikazi wa viwango tofauti pale kazini ikiwemo wenye vyeo. Tazama katika ubeti wa tatu mshororo wa kumi na tano katika wimbo wake Rusty Gee uitwao *Mihadarati;*

> …hata kama una cheo si unajitunza
> leo ulete maendeleo…

Wafanyikazi wenye nyadhifa kazini wanahimizwa kujitunza kwa kuepukana na uraibu wa mihadarati ili waweze kujiendeleza maishani. Maendeleo haya yao yalikuwa muhimu katika ukuaji wao na jamii kwa jumla. Wimbo huu ulilenga wafanyikazi hususan wale wenye vyeo mbalimbali kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya ili waweze kujiendeleza.

Dawa za kulevya pia ziliwaathiri vijana ambao walipaswa kuajiriwa ili kujenga taifa lao. Hali hii ilibainika katika ubeti wa pili mishororo ya kwanza, pili, tatu, sita, saba na nane katika wimbo wake Stivo Simple Boy uitwao *Mihadarati*;

> Unapata vijana, wameketi keti tu
> Wanavuta mihadarati, hawajali
> Wanapoteza wakati, hawana habari…
> …Wametulitulituli wamebaki jobless
> Kushoto na kulia manze wanalia hakuna kazi
> Wapate kazi, waishi vizuri…

Wimbo huu ulisawiri picha ya vijana waliopotelea katika uraibu wa mihadarati. Vijana hawa wanapoteza wakati wao katika uraibu wa dawa za kulevya bila ya kujali lolote ilhali walipaswa kuwa wanafanya kazi mbalimbali katika jamii ili kujenga taifa lao. Wenzao walio na uwezo wa kufanya kazi nao wanalalamika kwa kushindwa kupata nafasi za ajira na unyanyapaa huo unawasukuma katika uraibu wa mihadarati.

Heshima ni mojawapo ya kigezo muhimu katika jamii kwa mwanajamii yeyote yule. Heshima hutokana na matendo, maongezi na tabia zenye kukubalika katika jamii. Kwa upande mwingine, iwapo matendo ni kinyume na matarajio ya jamii mwanajamii huyo huwa haheshimiki kamwe. Hali hii ilijitokeza katika ubeti pili mishororo ya kwanza, saba na kumi na sita ya wimbo wake Rose Muhando uitwao *Pombe*;

> Heshima yako imeshuka…
> …Baba amelala mtaroni…
> …Baba unaitwa mzee wa ovyo…

Ubeti huu ulidokezea jinsi matumizi ya mihadarati yalivyoathiri waraibu wake katika jamii. Unywaji wa pombe wa kupindukia uliathiri mlevi alipolewa chakari katika jamii. Mlevi alipoteza heshima yake kwa kujidhalilisha kwa kulala mtaroni kwa kulewa chakari



DRAFT

kiasi kwamba alishindwa kutembea. Kitendo hiki cha kushindwa kutembea na kulala mtaroni miongoni mwa matendo mengineyo ya kudhahilisha yaliwafanya walevi kuitwa 'mzee wa ovyo' na wanajamii. Jina hili lilionyesha kwamba mlevi hakuheshimiwa katika jamii.

Mihadarati zinapotumika kwa muda mrefu zina athari kubwa kwa afya ya waraibu wake. Matumizi ya dawa za kulevya huwa chanzo cha magonjwa mbalimbali katika mwili wa mraibu na hatimaye hupelekea kifo. Vijana huiga mambo mengi ya kigeni kwenye mtandao, runinga na sinema na hili huchangia sana katika kuenea kwa magonjwa yakiwa ni pamoja na Upungufu wa Kinga Mwilini (Ukimwi) na mengine mengi ya zinaa (Kinyanjui, 2022). Hivyo basi, ni bayana kuwa uraibu wa dawa za kulevya ulihusiana na magonjwa katika jamii kama ilivyobainika katika nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

Uraibu wa mihadarati ulihusishwa na magonjwa katika nyimbo tatu (3) za kizazi kipya ambazo ni wimbo *Mihadarati* wake Stivo Simple Boy na ule wa Rusty Gee na wimbo *Pombe* wake Rose Muhando. Kwanza kabisa, unywaji wa pombe ulikuwa na madhara kwa afya ya walevi kama ilivyobainika katika ubeti wa kwanza mshororo wa tisa wa wimbo wake Rose Muhando uitwao *Pombe*;

> …Pombe ina magonjwa…

Kwa mijibu wa wimbo huu wanajamii wanaathirika kwa kupata magonjwa kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Magonjwa haya ni kama vile ugonjwa wa ini, saratani, uvimbaji wa kongosho, shinikizo la damu, magonjwa ya akili, kiharusi na ugonjwa wa moyo miongon I mwa magonjwa mengine. Wanajamii walipaswa kuepukana na uraibu wa pombe ili wawe wenye siha njema. Hatimaye, matumizi ya mihadarati pia yalikuwa na athari kubwa katika afya ya wanawake katika jamii. Tazama ubeti wa tatu mshororo wa nne katika wimbo wake Rusty Gee uitwao *Mihadarati;*

> Madawa ya kulevya yanaathiri nguvu
> za kike,
> Nanyi jiekeni huru, sije kosa Watoto
> kwa sababu ya anasa

Wanawake wanahimizwa kuepukana na anasa haswa kwa kujihusisha na uraibu wa dawa za kulevya katika jamii. Uraibu wa dawa za kulevya uliwaathiri wanawake katika jamii kwa kukosa nguvu za kike. Athari hii ilikuwa changamoto kubwa kwao kupata watoto baadaye. Wimbo huu umelenga kuwaonya wanawake kuepukana na matumizi ya mihadarati ndiposa wawe na uwezo wa kujifungua watoto siku za usoni. Nyimbo hizo tatu za kizazi kipya zilishikilia kwamba uraibu wa dawa za kulevya una madhara katika jamii kwa kusababisha magonjwa kwa waraibu. Taasisi ya ndoa pia iliathirika na matumizi ya mihadarati katika jamii. Usherati ulijitokeza katika nyimbo za kizazi kipya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Hili lilijitokeza katika ubeti wa pili mshororo wa kumi na mbili katika wimbo wake Rose Muhando uitwao *Pombe*;

> …Kumbe kupepesapepesa baba yupo
> mpango wa kando…

Kutokana na unywaji wa pombe, wanaume wanajihusisha kwa mahusiano nje ya ndoa zao. Mahusiano haya yaliwafanya kukosekana nyumbani kwao huku familia zao zikihangaika. Matumizi haya ya mihadarati yalisababisha uzinifu katika jamii na hivyo yalipaswa kuepukwa. Nyimbo za kizazi kipya pia ziliangazia jinsi matumizi ya dawa za kulevya huchangia kwa visa vya ubakaji katika jamii. Hali hii inajitokeza katika ubeti wa pili mshororo wa tatu wa wimbo wao Domani Munga na SewerSyda uitwao *Mihadarati*;

> …Plenty vices, ndio maana approach
> ni marijuana
> Niaje yout ako 25 akarape shosh wa
> 91?...

Mshororo huu unarejelea kisa cha kijana wa miaka ishirini na mitano (25) kumbaka nyanya wa miaka tisini na moja (91). Kinaya hiki ni kutokana na tofauti yao ya umri kuashiria athari mojawapo ya uvutaji bangi. Matumizi haya ya mihadarati yaliwapotosha vijana katika jamii kwa kujiingiza katika visa kama ubakaji katika jamii.

Madhara mengineyo ya uraibu wa dawa za kulevya zilijitokeza katika wimbo wake Rose Muhando uitwao *Pombe* hususan katika familia. Kwanza kabisa, uraibu wa mihadarati ulichangia katika kuvunjika kwa familia, kukosekana kwa mapenzi katika katika familia,



DRAFT

kupotea kutoka nyumbani, kutokidhi mahitaji ya boma kama vile, mavazi kwa mama kuvalia nguo zilizochanika chakara chakara, kukosa chakula na kushinda njaa, karo ya wanawe kutolipwa na mwenye nyumba kudai kodi ya nyumba. Hali hii ilitokana na baba kupotelea kwa unywaji wa pombe wa kupindukia unaomfanya kutelekeza majukumu yake nyumbani.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Makala haya yameonyesha kuwa nyimbo za kizazi kipya mtandaoni zilikuwa na mchango mkubwa katika vita dhidi ya uraibu wa dawa za kulevya. Kupitia nyimbo za kizazi kipya katika mtandao wa kijamii wa *YouTube*, athari za uraibu wa mihadarati ziliweza kubainika moja kwa moja. Matokeo yalionyesha kwamba matumizi ya mihadarati yalikuwa na madhara kwa jamii, familia na waraibu wa dawa tofauti za kulevya kama njia mojawapo ya kuhamasisha jamii katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Nyimbo za kizazi kipya zilitumika kupinga matumizi ya mihadarati katika jamii kwa kuangazia athari za dawa za kulevya ili kutahadharisha jamii dhidi ya uraibu wa mihadarati. Athari hizi zilikuwa ni kusababisha wendawazimu, vifo, kufutwa kwa kazi kupitia nyimbo za kizazi kipya mtandaoni. Isitoshe, uraibu wa dawa za kulevya pia ulisababisha ukosefu wa maendeleo licha ya kuwa na cheo kazini, vijana kuwa mabwege, ukosefu wa heshima, magonjwa, uzinifu na ubakaji kama ilivyosawiriwa katika nyimbo za kizazi kipya mtandaoni.

Hatimaye, matumizi ya mihadarati ya kupindukia hususan pombe yaliathari familia kwa kutelekezwa kwa majukumu nyumbani kama vile kununua kwa chakula, mavazi, kulipa karo, kulipia kodi ya nyumba na kutokuwepo nyumbani. Athari hizi za pombe zilisawiriwa na watunzi wa kupitia nyimbo za kizazi kipya na lengo la kuhamasisha jamii dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni.

**Mapendekezo:** Makala haya yanapendekeza kwamba haja ipo ya mitandao mbalimbali tofauti na ule wa *YouTube* kutafitiwa kwa kurejelea athari za dawa za kulevya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Pili, ni vyema kuchunguza athari ya uraibu wa mihadarati kwa kurejelea aina nyinginezo za nyimbo mbali na zile za kizazi kipya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya mtandaoni. Hatimaye, athari za mihadarati pia zitafitiwe katika tanzu nyingine za fasihi pepe kama vile vichekesho, filamu na vipindi vya runinga kwa kurejelea suala la dawa za kulevya katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

## MAREJELEO


Atwoli, L., Mungla, P. A., Ndung'u, M. N., Kinoti, K. C., & Ogot, E. M. (2011). Prevalence of substance use among college students in Eldoret, western Kenya. *BMC Psychiatry*, *11*(1). https://doi.org/10.1186/1471-244x-11-34

Burns, R. B. (2000). *Introduction to Research Methods*. SAGE.

Chen, M. J., Miller, B. A., Grube, J. W., & Waiters, E. D. (2006). Music, substance use and aggression. *Journal of Studies on Alcohol, 67*(3), 373–381. https://doi.org/10.15288/jsa.2006.67.373

Jumbe, A. H. (2015). *Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Kizazi Kipya: Mfano kutoka katika Nyimbo za Mapenzi za Waimbaji Inspekta Haroun na Mwanafalsafa*. Chuo Kikuu cha Dodoma. https://shorturl.at/mGnRS

Kaithuru, P. N., Stephen, A., & Wanjiru, V. N. (2015). Alcoholism and its impact on work force: A case of Kenya Meteorological Service, Nairobi. *International Journal of Education and Research, 3*(1), 561–568. https://shorturl.at/l178V

Kaniki, O. T. N. (2019). *The Effects of Drug and Substance Abuse on Employees' Job Performance on Selected Insurance Companies in Nairobi, Kenya*. United States International University-Africa. https://erepo.usiu.ac.ke/11732/5259

Kinyanjui, M. W. (2022). Alcohol Consumption among Employees: A Case of Selected Companies in Nairobi County. *Usiu.ac.ke*. http://erepo.usiu.ac.ke/11732/7176

Koech, L. K. (2021). Relationship between Watching "Gengetone" Music and Drug Abuse among the Youth in Uasin Gishu County, Kenya. *East African Journal of Interdisciplinary Studies*, 3(1), 103–115. https://doi.org/10.37284/eajis.3.1.312

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques* (2nd ed.). New Age International.

Kristin, G. E. (2002). *Qualitative Methods in Social Research*. McGraw-Hill.

Massoud, I. A. E. (2018). *Kuchunguza Nafasi ya Mwanamke katika Tamthilia ya Alikiona* (Unpublished doctoral thesis). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mbeere, C. K. (2022). *Usawiri wa Dawa za Kulevya katika Matini Teule za Fasihi ya Watoto ya Kiswahili* (Unpublished master's thesis). Chuo Kikuu cha Chuka.

McLuhan, M. (1964). *Understanding Media: The Extensions of Man*. McGraw-Hill. https://designopendata.wordpress.com/wp-content/uploads/2014/05/understanding-media-mcluhan.pdf

Mihalis Kuyucu. (2015). The Effects of Media on the Music Listening Habits of the University Students in Turkey. *International Conference Management, Economics, Business and Social Sciences and Humanities Research (ICMHRCon), 15-16 January 2015, Istanbul Turkey.* https://www.researchgate.net/publication/303899194_The_Effects_of_Media_on_the_Music_Listening_Habits_of_the_University_Students_in_Turkey

Motyka, M. A., & Ahmed, A. (2019). Musical preference and drug abuse among youth: An empirical study. *Research and Advances in Psychiatry,* 6(2), 50–57. https://www.researchgate.net/publication/336847336_Musical_preference_and_drug_use_among_youth_an_empirical_study

Mukandabvute, A. A., & Gores, M. (2021). Athari za kimaadili zitokanazo na nyimbo za muziki wa Singeli nchini Tanzania. *Mulika, 40*(2), 95–108. https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/4731/4068

Musembi, N. (2016). *Mabadiliko ya Maudhui katika Nyimbo za Jando: Mfano kutoka Jamii ya Wakamba* (Unpublished doctoral thesis). Chuo Kikuu cha Mount Kenya. http://erepository.mku.ac.ke/handle/123456789/5488

Norah, G. (2017). *Uchambuzi Linganishi Wa Fani Na Maudhui Ya Nyimbo Za Harusi Za Kimeru Na Za Kiswahili*. Uonbi.ac.ke. https://erepository.uonbi.ac.ke/items/f8accab1-a3cb-4877-944d-6d160b52c782

Nyamemba, R. (2015). *Uchanganuzi Linganishi Wa Maswala Ya Vijana Na Jinsi Yanavyoshughulikiwa Na Waandishi Katika Diwani Ya Tunu Ya Ushairi*. Uonbi.ac.ke. https://erepository.uonbi.ac.ke/items/3941b615-7173-4926-834e-0eb320e87ba1

Ogechi, O. N. (2024). *Taratibu za Kuendesha Utafiti na Masuala Mengine*. The Jomo Kenyatta Foundation.

Resnik, D. B. (2021). *Ethics and the Responsible Conduct of Research* (3rd ed.). Springer. https://shorturl.at/t8bZv

Ruhweza, I. (2018). *Impact of Broadcasting Media in Fighting Against Drug Abuse in Uganda: A Case Study of NBS Television, Kampala* (Unpublished degree thesis). Kampala International University. https://ir.kiu.ac.ug/bitstream/20.500.12306/6860/1/Ruhweza%20Ibrahimu.pdf

Schechner, R. (1985). *Between Theatre and Anthropology*. University of Pennsylvania Press.

Stringer, E. T. (2007). *Action Research* (3rd ed.). SAGE. https://cmn-cdn-001.sagepub.com/books/titles/275393/att_sb1_141645.pdf

United Nations Office on Drugs and Crime. (2016). *World Drug Report 2016* (Sales No. E.16.XI.7). https://www.unodc.org/doc/wdr2016/WORLD_DRUG_REPORT_2016_web.pdf

United Nations Office on Drugs and Crime. (2022). *World Drug Report 2022: Executive Summary – Policy Intervention No. 1.* United Nations. https://digitallibrary.un.org/record/3984478

Valkenburg, P. M., Peter, J., & Walther, J. B. (2016). Media effect: Theory and research. *Annual Review of Psychology, 67*, 315–338. https://doi.org/10.1146/annurev-psych-122414-033608

World Health Organization. (2019). *Global Status Report on Alcohol and Health 2018*. World Health Organization. https://www.who.int/publications/i/item/9789241565639